# Watu Wote Wanatakiwa Kufahamu Nini Kuhusu Maandiko?



# "Biblia Ni Nini?"

Neno "Biblia"
Linatoka kwa lugha
Ya Ki-yunani, na
Maana lake ni
"Vitabu".



Ni kusanyiko la vitabu
Vidogo sitini na sita kuhusu **Mungu**.

## Na Biblia inamagawanyiko mawili





**Agano la Kale ina maadithi kuhusu mapatano ya zamani kati ya Mungu na Wanadamu. Hasa Waebrania (Wayahudi) baada ya kupata uhuru kutoka utumwa katika nchi ya Misri.....na jinsi Wayahudi walifuata maagizo yake.**

**Agano Jipya ina maadithi kuhusu mapatano mapya kati ya Mungu na Wanadamu Wote. Na Agano Jipya inaeleza matokeo kuhusu kuzaliwa, maisha, kifo na ufufuo wa Yesu....Aliyefungua uhusiano na Mungu kwa watu wote, ambao wako tayari kuamini na kubatizwa kwa ajili ya dhambi zao.**



**Nani** Aliandika Biblia?

**Biblia iliandikwa na waandishi wengi, kama 40, na wengi walikuwa Waebrania, waandishi wengine hatuelewi.**

**Lini** Iliandikwa?

**Wakati tofauti, katika kipindi cha miaka 1,600, 1500 KK—96 BK.**

Iliandikwa **Wapi?**

**Mahali mengi Tofauti— Palestina, Babeli, Misri, Rumi, Antioki, Patimo nk.**

**Kwa Nini** Iliandikwa?

**Kwa makusudi mengi—kufundisha kuhusu Mungu na njia zake, kwa kutangaza Kanisa la Yesu.**

Nani **Alichagua** maandishi haya?

**Kundi la mwanateolojia, waliposanyika Nicaea mwaka wa 325 BK.**

**Kwa Nini** Tusome Biblia?

**Kwa makusudi mengi—**

**Ili uelewa Mungu na kazi zake.**
**Ili ujua jinsi ya kuishi na matendo mazuri.**
**Ili tujifunza kwa mifano mengi ya watu mbali mbali.**
**Ili tufahamu Kristo na njia zake.**
**Ili tufahamu mengi kuhusu kitabu kinachofahamikwa zaidi ya viatbu vyote hapa ulimwenguni.**

# Agano La Kale

**(Maandiko Kwa Waebrania)**



**Agano La Kale**
**Ni vitabu 39 vya Historia ya Wayahudi na Baba zao. Vitabu vile vimeandikwa hasa kwa lugha ya Ki-Ebrania na vinahusu:**

1) **Historia ya mashujaa na matokeo**
2) **Sheria**
3) **Mahubiri maluumu**
4) **Waandishi wa kujipima.**
5) **Mashairi.**

**Agano la Kale yote yali-lekea kazi ya Yesu na Agano Jipya, Gal. 3:23-27.**

**Vitabu 5 Vinahusu Sheria (Torati).**

*Mwanzo*
*Kutoka*
*Mambo ya Walawi*
*Hesabu*
*Kumbukumbu La Torati*

**Vitabu 18 Vinahusu Historia, Filofisia Na Mashairi**

Yoshua
Waamuzi
Ruth
1 Samweli
2 Samweli
1 Wafalme
2 Wafalme
1 Mambo ya Nyakati
2 Mambo ya Nyakati
Ezra
Nehemia
Ayubu
Zaburi
Mithali
Mhubiri
Wimbo Ulio Bora
Maombolezo

**Vitabu 16 Vinahusu Manabii**

Isaya
Yeremiah
Ezekieli
Danieli
Hosea
Yoeli
Amosi
Obadia
Yona
Mika
Nahum
Habukuki
Zefania
Haggai
Zekaria
Malaki

**Vitabu tano vya kwanza vinahusu:** **"Sheria" ("Torati")** { Pia vinaitwa "Pentatui" au "Vitabu Vitano Vya Musa"

| | | |
|---|---|---|
| **1 MWANZO** | —Jinsi ulimwengu uliaanza.<br>—Historia ya Awali ya Wanadamu<br>—Mwanzo wa Wayahudi na nafasi yao wa kuwa "Waliochaguliwa" na Mungu. | Sura 50<br>1-11: Historia ya Wanadamu<br>39 ziliofuata Historia ya Mababa, na Baba za Waebrania: **Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yusufu.** |
| **2 KUTOKA** | —Jinsi Waisraeli walikimbia kutoka Misri.<br>—Sheria waliowapa kushika wa kati walifanya agano (mapatano) na Mungu kule Ml. Sinai. | Sura 40<br>1-18: Historia<br>22 zilizofuata Sheria, na mapatano kati ya Mungu na Waisraeli (Sheria Kumi). |
| **3 MAMBO YA WALAWI** | —Sheria nyingi sana zimeongezeka.<br>—Sheria nyingi kuhusu Matoleo.<br>—Jinsi ya kushika Sikukuu. | Sura 27<br>1-7: Sheria za Sadaka<br>3 zilizofuata: Kutakasa Makuhani<br>6 zilizofuata: Vitu "Chafu" vitu "Safi"<br>11 zilizofuata: Sheria za Utukufu. |
| **4 HESABU** | —Musa alihesabu watu mara mbili.<br>—Adhithi za Wana WaIsraeli Walipotangatanga Jangwani. | Sura 36<br>1-4 na 26: Mahesabu ya Wanadamu.<br>Sura zilizobaki: Historia |
| **5 KUMBUKUMBU LA TORATI** | —Musa alirudia Kutanganza na Kutoa Sheria kwa mara ya pili.<br>— | Sura 34<br>1-11: Hutuba Ya Musa<br>12-26 na 29: Kurudia Sheria<br>Kitabu hiki kwa Ki-Yunani ni "Sheria ya Pili". |



# Vitabu 18 Vya
# Historia, Filosafia na Mashairi

| | | |
|---|---|---|
| **6** Yoshua<br>Adithi ya Yoshua aliyechukua nafasi ya Musa kuwa kiongozi wa Israeli na kuvamia nchi ya Kanaani | **7** Waamuzi<br>Gugu ilitokea katika Nchi ya Ahadi, kila mtu aliaanza kufanya kama alivyotaka. Walipotea Umoja wa Mataifa, waliongozwa na Waamuzi. | **8** Ruth<br>Adithi ya upendo, jinsi Mmoabu alichagua Mungu na watu wake, na akawa mhenga wa Mfalme Daudi. |
| **9** I Samweli<br>Mwisho wa Waamuzi na chanzo cha uongozi wa ufalme chini ya Mfalme Sauli, mfalme wa kwanza wa Israeli. Mpaka Sauli alikufa. | **10** II Samweli<br>Kinaendeleza habari kuhusu Israeli baada ya kifo cha Sauli. Daudi alichaguliwa kuwa mfalme mpya, pia tunasoma kuhusu utwala wake mpaka mwaka wake wa mwisho. | **11** I Wafalme<br>Daudi alikufa na utawala wa Sulemani mtoto wa Daudi na Bethsheba. Sulemani alijenga hekalu na nyumba yake. |
| **12** II Wafalme<br>Nchi ya Israeli iligawanyika kuwa mataifa mawili: Israeli na Yuda. Nchi zote mbili zilitekwa na Maadui kwa sababu ya uovu. | **13** I Mambo ya Nyakati<br>Historia kutoka mwanzo mpaka Mfalme Daudi alikufa. | **14** II Mambo ya Nyakati<br>Historia ya Nchi ya Israeli toka kwa Daudi mpaka Yuda ilitekwa na Babeli katika mwaka wa 586?. |
| **15** Ezra<br>Adithi kuhusu marejesho ya Waisraeli kutoka Babeli chin ya Kyrus, Mfalme wa Uajemi katika mwaka wa 536?. | **16** Nehemia<br>Adithi kuhusu kiongozi muhimu sana Nehemia, jinsi aliaacha kazi yake katika baraza ya Ujemi kwa kujenga upya mji wa Daudi. | **17** Esta<br>Adithi ya Mke wa Mfalme wa Uajemi na alikuwa Myahudi, jinsi aliokoa watu wake. Katika kitabu hiki Mungu hajatajwa. |
| **18** Ayubu<br>Adhithi kuhusu jinsi ni lazima watu wazuri wateswa pia. | **19** Zaburi<br>Nyimbo za sifa na maombi 150. Mengi ni ya Mfalme Daudi. | **20** Mithali<br>Kusanyiko ya mithali ya dini na ya ulimwengu huu. Zimetoka kwa Sulemani na watu wengine. |
| **21** Mhubiri<br>Mtazamo wa Maisha zilikanusha na Mfalme Sulemani | **22** Wimbo Ulio Bora<br>Wimbo wa Upendo uliandikwa na Sulemani. Wengi wanaamini wimbo huu ni mfano wa Upendo wa Mungu au upendo wa Kristo. | **23** Maombolezo<br>Wimbo wa Maziko kuhusu maagamizo ya Yerusalemu. Wakati Wababeli walitekwa mji kwa sababu Wairaeli walimuasi Mungu. |

## Vitabu 16 Vya Manabii (Unabii)

Vingi vinahusu Historia na mahubiri

| | | | |
|---|---|---|---|
| **24**<br>Isaya<br>Mahubiri ya Nabii Isaya. Yanaohusu Utoba na kuja kwa Mwokozi na Ufalme Mpya. | **25**<br>Yeremia<br>Unabii na maombi ya Mhubiri maalumu, kwa kipindi cha miaka 40. Alihubiri toba, lakini walikaaa kumsikia. | **26**<br>Ezekieli<br>Maneno ya Unabii na Tuamini, kutoka kwa mkuhani kwa waliotekwa Babeli. | **27**<br>Danieli<br>Adithi ya Kijana aliye-toka Yuda lakini kwa sababu ya utumwa aliishi chini ya Mfalme wa Ba-beli. Alitabiri kuhusu Yesu na Ufalme Wake. |
| **28**<br>Hosea<br>Kitabu Cha Kwanza cha manabii madogo. Ali-hubiri kwamba Mungu ata-samehe watu kama wata-juta na kutubu dhambi zao. | **29**<br>Yoeli<br>Kitabu cha Mahubiri kuhusu hukumu juu ya Yuda. | **30**<br>Amosi<br>Mahubiri ya kwanza yali-yotunzwa na wanadamu. Alihubiri kwa Israeli baada ya kugawanyika na Yuda. Alihubiri hukumu kwa ajili ya dhambi zao. | **31**<br>Obadia<br>Mahubiri kwa kulaumu Nchi ya Edomu (Ishmali) kwa kujiunga na maadui ya Yuda. |
| **32**<br>Yona<br>Adithi ya Nabii Yona. Mungu alimtuma aenda kuhubiri kwa Waashuru. Kitabu hiki kinaonyesha Mungu anapenda watu wote. | **33**<br>Mika<br>Mahubiri ya Nabii ndani ya Yuda: alijumlisha mawazo ya Amosi, Hosea na Isaya. | **34**<br>Nahum<br>Mahubiri kinyume na Asshuru baada ya Asshuru kuvamia Yuda. | **35**<br>Habakuki<br>Nabii aliyefanya kazi Yuda karibu na wakati wa Nahum, alihubiri kinyume na Wababeli. |
| **36**<br>Zefania<br>Mahubiri ya kujenga imani ya Waisraeli baada ya ua-gamizo wa Yerusalemu katika 586 kk. | **37**<br>Haggai<br>Alihubiri kwa Wayahudi walipopata nafasi ya ku-rudi nyumbani baada ya utumwa chini ya Babeli. Alisitiza sana ujenzi wa Hekalu la Mungu. | **38**<br>Zekaria<br>Alisharekea kazi ya Hag-gai kwa kutoa juhudi ya kujenga tena Hekalu. | **39**<br>Malaki<br>Maana yake ni “Mjumbe Wangu”. Alilaumu Waisraeli kwa kurudi kwenye dhambi na alitabiri kuhusu yule atajiandaa njia kwa |

## Biblia inaongea kuhusu zaidi ya miaka 2000 ya Historia ya Wanadamu.

**1900 KK—96 BK**

"KK" maana yake ni kabla ya Kristo. "BK" maana yake ni baada ya Kristo.

| | |
|---|---|
| **1900-1700 K.K.** | **Kipindi Cha Mababa**<br>**Ibrahimu**<br>**Isaka**<br>**Yakobo na Yusufu**  |
| **1700-1500 K.K.** |  **Kipindi Wana wa Israeli Walipoiishi Goshen, Misri. Walifanyikiwa Sana!** |
| **1500-1300 K.K.** | **Kipindi hiki Wana Waebrania waliishi Misri pia, lakini waliteswa sana.**  **Wana wa Israeli, Waebrania, Watoto wa Yakobo ni mamoja.** |
| **1300-1200 K.K.** |  **Baada ya kupiga Wamisri na mapigo kumi, Musa na Mungu walichukua Uhuru kwa**<br>**Waebrania, na wakachukua Palestina.** |
| **1200-1000 K.K.** | **Kipindi cha Waamuzi. Mungu aliongoza Israeli kupitia Waamuzi. Lakini watu wa Israeli walianguka kwenye ibada ya sanamu. Kipindi hiki kili kuwa kipindi cha uovu sana katika nchi ya Israeli.**  |

**1000-900 K.K.**

**Ufalme Wa Waebrania**
**China ya Sauli, Daudi na Sulemani.**



**900-721 K.K.**

**Ufalme Mbili Wa Waebrania**
**Kusini—Yuda**
**Kasikasini—Israeli**

**721-586 K.K.**

**721-Israeli**
**Ilitekwa na Waashuru na ikawa "Makabila kumi yaliyopotea."**

**Yuda**
**612-Maangamizi ya Ninawi**
**608-Walitawala na Misri**
**605-Walitawala na Wababeli**
**597-Yerusalemu ilitekwa**
**586-Maangamizi ya Yerusalemu**

**586-537 K.K**

**Utumwa**
**Kule Babeli**

**536-333 K.K.**

**Walitawala na Waejemi**
**537-Wengi walirudi kutoka Babeli**
**516-Wakajenga hekalu la pili**
**444-Nehemiah alikuwa Govana**
**397-Ezra alikuwa Mwandishi**
**333-Walitekwa na Alexander Mkuu.**



**333-142 K.K.**



**Walitawaliwa Na Waunani**
**333-142**
**Alexander Mkuu, Ptolemy Logi, Seluciusi**

**142-62 K.K.**

**Walitawalia na Makabayo**
**Makabayo walikuwa makuhani na wafalme**
**142-62 K.K.**



# 63 K.K. –96 B.K.
# Walitawaliwa na Warumi

***Katika Utawala Wa Rumi....***



**Yesu Kristo alizaliwa**

**Hapa ulimwenguni alitengenza njia kwa ajili ya Kanisa. Alichaguwa mitume 12 kumsaidia yeye katika kazi yake.**

**Petro**
**Andrea**
**Yakobo**
**Yohana**
**Filipo**
**Tomaso**
**Mathayo**
**Bartholomu**
**Yakobo**
**Thadayo**
**Simon**
**Yudas**

***Pia.....***



**Kama mwana kon-doo, Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, Yoh. 3:16.**



***Na.....***



**Kwa sababu ya mauti yake, amenunua Kanisa, Mdo. 20:28. Na Mitume wake, wote wakafungua Kanisa katika siku ya Pentokosti katika kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya 2.**

**Na wote siku ile walioin-gia katika Kanisa, wali-tubu dhambi zao halafu waka batizwa (zamisha) kwenye maji. Hii ndio njia ya peke ya kuingia katika Kanisa. Mungu hakutoa njia ya pili.**

***Matokeo mengine muhumi.....***

**Yesu alimwita Pauli kuhubiri kwa mataifa.**
**Wakristo wakateswa sana kwa sababu ya imani yao.**
**Pauli aliuawa kule Rumi. 63-64**
**Wayahudi walimuasi Rumi 66-70.**
**Tito, mgeradadi kutoka Rumi ali haribu hekalu na kuagamiza Yerusalemu.**
**Agano Jipya yote yakaandika 40-96 B.K.**

# Nchi Ya Yesu



# Agano Jipya

(Maandiko Kwa Wakristo)



**Agano Jipya**

**Ni kusanyo ya vitabu 27 viliandikwa katika lugha ya Kiyunani katika kipindi cha karibu na miaka sitini, baada ya Kristo. Ni vitabu vile ni Viongozi vya Wokovu, vinafundisha Injili, na vinatangaza Kanisa la Kristo. Jinsi siku moja Mungu atafuta ulimwengu huu na kupeleka watu wote waminifu waenda kukaa naye kwa milele mbinguni.**

**Angalia: Kuna mistai mengi zimerudi kwenye Agano la Kale lakini sasa zimeandikwa kwa Roho Mpya.**

| | |
|---|---|
| **Vitabu Vinne Vya Kwanza Vinaiitwa "Vitabu Vya Injili"** | **Mathayo<br>Marko<br>Luka<br>Yohana** |
| **Kitabu Kimoja kinzumgumza matendo ya Mitume, hasa Petro na Paulo.** | **Matendo Ya Mitume** |
| **Barua 13 Za Paulo Kwa makusanyiko na watu** | **Warumi<br>1 Wakorinto<br>2 Wakorinto<br>Wagalatia<br>Waefeso<br>Wafilipi<br>Wakolosai<br>1 Watheso-lanica<br>2 Watheso-lanica<br>1 Timotheo<br>2 Timotheo<br>Tito<br>Filimon** |
| **Barua Zingine 8 Za Kujenga Wakristo Wapya** | **Waebrania<br>Yakobo<br>1 Petro<br>2 Petro<br>1 Yohana<br>2 Yohana<br>3 Yohana<br>Yuda** |
| **Kitabu Cha Mwisho Ni kitabu cha Maono** | **Ufunuo** |

# Vitabu Vya Injili

Maana ya neno "injili" ni "habari Njema"

**Vitabu Vya Injili Vinahusu, Kuzaliwa, Utoto, Mafundisho, Kifo, Na Ufufuo Wa Yesu Kristo.**

**Mathayo**

-Kimeandikwa karibu na mwaka wa 50 B. K., na kilichapishwa baada ya uagamizo wa Yerusalemu (70 B. K.)
-Kimeandikwa kwa ajili ya Wayahudi. Na kimeandkiwa ili Mathayo aonyesha kwamba Yesu alitimiza unabii kuhusu Mesia.

**Marko**

—Kimeandikwa kabla ya Injili zote.
—Kimeandikwa karibu na mwaka wa 50 B .K., na kilichapishwa baada ya kuanguka kwa Yerusalmu.
—Kimeandikwa kwa kuthibitisha kwa Warumi kwamba Yesu, aliyekufa msalabani alikuwa Mwana wa Mungu.

**Luka**

-Maelezo ya 33% ni sawa na kitabu cha Marko.
-Kitabu hiki kimeandikwa kwa ajili ya Wayunani.
-Kitabu hiki kilithibitisha Yesu alikuwa Mwokozi wa ulimwengu huu kwa watu wote kwa milele.
-Vitabu vitatu vya kwanza pia vinaiitwa "**Synoptics**" kwa maana vimeandika kuhusu adithi zile zile.

**Yohana**

—Kiliandika kwa kuongozo Kanisa la awali.
—Kinaongelea kuhusu Filosofia na siri za Neno la Mungu.

# Kitabu Cha Matendo ya Mitume

## Maelezo ya Dini Mpya

Maelezo ya peke kuhusu mwanzo wa Ukristo.
Maeleo yanaohusu jinis Injili ilipelekwa kutoka Palestina mpaka Rumi, mji mkuu wa ulimwengu.
Kitabu cha pili cha Luka, aliyeandika Injili ya Luka.
Kinaeleza muda ya miaka 30 baada ya kifo cha Yesu.
Kina sura 28.
Sura ya 1 –12 zilitokea Palestina.
Sura 13-28 zilihusu safari za mmisionari Paulo alipotembea
Yudea, Samaria, na kupita Imara ya Rumi, mpaka alipofungwa Rumi.



# 13
# "Barua Za Paulo"

**Ailianzika kwa makanisa na kwa watu binafsi.**
**Na ziliandika miaka 20-35 baada ya kifo cha Yesu Kristo.**

6
Barua Kwa
**Warumi**
Iliandikwa kule Korinto kwa ajili ya Kanisa kilikuwepo Rumi.
Aliandika kwa sababu:
Alitaka Wakristo waache kuchanganya mambo ya kale na ya Kristo.

7
Nyraka ya Kwanza Kwa
**Wakorinto**
Paulo aliandika kitabu hiki iliasahisha matatizo ya Ubinafsi, ya Ibada, na matatizo yaliohusu Roho Mtakatifu.
57-58 B. K..

8
Nyaraka ya Pili Kwa
**Wakorinto**
Aliandika ili aone mabadiriko yaliyotokea baada ya kutuma barua ya kwanza.
Pia alionya waovu,
57-58 B.K.

9
Barua Kwa
**Wagalatia**
Aliomba wakristo wa Galatia, wasirudi nyuma na kushika mambo ya Agano la Kale,
57-58 B.K.

10
Barua Kwa
**Waefeso**
Barua kwa Wakristo wote wa Asia Ndogo kuhusu umoja wa Kanisa na ukubwa wa Yesu,
62-63 B.K.

11
Barua Kwa
**Wafilipi**
Paulo aliandika alipofungwa Rumi. Alitoa shukurani kwa msaada alipokea kutoka kwa Kanisa la Filipi na alionya wakristo kuhusu walimu wa uongo,
62-63 B. K.

12
Barua Kwa
**Wakolosai**
Aliandika kwa sababu ya matatizo mengi yaliyohusu mambo ya
Teolojia,
62-63 B. K.

13
Nyaraka ya Kwanza Kwa
**Wathesalonike**
Aliandika kitabu hiki wakati alikuwa Korinto kwa mara ya kwanza. Alikuwa na kutoa shukurani kwa Wathesalonike kwa sababu ya repoti alisikia kutoka kwa Timotheo,

14
Nyaraka ya Pili Kwa
**Wathesalonike**
Alikuwa na kufundisha vizuri kuhusu tabia na mawazo yao kuhusu kurudi kwa pili kwa Yesu Kristo,

52-53 B.K.

15
Nyarka ya Kwanza Kwa
**Timotheo**
Aliandika baada ya kufunga mara ya kwanza Rumi, na alishauri Timotheo jinsi ya kupambana na mawazo mabovu ya Waefeso,
66-67 B.K.

16
Nyraka ya Pili Kwa
**Timotheo**
Aliandika wakati alifungwa Rumi kwa mara ya pili. Aliomba kuonana na Marko kabla ya kifo chake na alieleza upendo wake juu ya Timotheo.
65-67 B.K.

17
Barua Kwa
**Tito**
Aliandika kabla aliandika barua za Timotheo. Na alimsharui Tito jinsi ya kuendesha Kanisa pale Krete,
65-67 B. K.

18
Barua Kwa
**Filemoni**
Onesmo, mtumwa wa Filemoni alitoroka na alimkuta Paulo Rumi. Aliposikia Injili alibatizwa na aliamua kurudi kwa Filemoni. Paulo aliomba Filemoni awe mpole na aonyesha

Na Barua
8
Zingine



19

Baura Kwa

**Waebrania**

Haileweki nani aliandika kitabu hiki, watu wanakisia Paulo, Apolo au Timotheo.
Habari zinaeleza ubora wa Agano Jipya na mwandishi aliwashauri wakristo watii Mungu kwa moyo wote.

66 B. K.

20

Barua Kutoka Kwa

**Yakobo**

Inawezekana mdogo wake Yesu aliandika kitabu hiki.
Yakobo alikuwa mtakatifu aliyeishi Yerusalemu na aliwasaidia kuongoza wakristo wapya ili waishi maisha bora.
Maneno yake yanatufundisha jinsi ya kuishi tofauti na ulimwengu huu,

21

Barua ya Kwanza Kutoka Mkono Wa

**Petro**

Aliandika kwa Makusanyiko ya Kanisa la Kristo Asia Ndogo.
Alitaka kujenga na kuimarishe wakristo ili wasianguka kwa sababu ya mateso makali,

64 B.K.

22

Barua ya Pili Kutoka Mkono Wa

**Petro**

Alirudia mambo yale yale aliyetamka katika barua yake ya kwanza. Tena alikuwa na wafariji wakristo kwa kuongea kuhusu kurudi kwa mara ya pili ya Yesu Kristo,

64—66 B. K.

23, 24, 25

Barua za Kwanza, Pili na Tatu Kutoka Mtume Aliyependwa Na Yesu Kuliko Wote

**Yohana**

Aliandika kuhusu usafi wa roho, upendo wa ndugu, walimu wa uongo na mambo mengi ya Theolojia.

Haileweki barua ziliandika lini. Inawezekana baada ya kuanguka kwa Yerusalemu.

26

Barua Ya

**Yuda**

Alikuwa mdogo wa Yakobo.
Na aliandika kitabu hiki kwa wakristo waliolegea nyuma na walianza kufuata mambo ya upagani tena.

66-80 B. K.

27

Na Kitabu Cha Mwisho Wa Biblia Ni

**Ufunuo**



Habari zinahusu jinsi Yesu kama mwana kondoo ni uhai na jinsi Mungu ataweka kila kitu kiwe sawa.
Kitabu hiki ni kitabu cha ishara, kwa kuonyesha kwamba Mungu ndiye anayetawala, na atalipiza kisasi juu ya wale waliteswa Wakristo wa awali, 96 B.

**Baadhi ya Mawazo Kwa Kusaidi Wewe Iliuelewi Biblia.**

| | |
|---|---|
| 1<br><br>Unahitaji kuwa na kiu na njaa kwa ajili ya haki, Mat. 5:6; Isa. 55:1; 65:13. | 2<br><br>Ni lazima upanga muda kila siku kwa kusoma maandiko, 2 Tim. 2:15. |
| 3<br><br>Ni lazima usome kitabu ki-moja wakati moja tu! Vitabu vingi unaweza kusoma chini ya saa moja, 1 Kor. 14:40. | 4<br><br>Soma Agano Jipya kwanza, kuanzia Injili mpaka Matendo hadi barua za Paulo na barua zingine, 2 Pet. 1:3; Ebr. 8:7-13. |
| 5<br><br>Jaribu kuelewa kusudi kwa kuandikwa kila kitabu. Fikiri kuhusu mwandishi, kwamba alikuwa nani na kwa nini alieleza yote? | 6<br><br>Pia jaribu kuelwa barua vi-tabu vilandikwa kwa wanani? Na maelezo yale kuwa na maana gani? |

| 7 | 8 | 9 |
|---|---|---|
| Kumbuka hatuna uwezo wa kutafsiri maandika kama tunavyopenda, 2 Pet. 1:19-21. | Pia andika mambo ulijifunza katika daftari. Na andika maswali, na mawazo yale muhimu yanauwezo wa kusaidia ukristo wako, 2 Tim. 3:16-17. | Kama unataka kuwa mwanafunzi mzuri wa maandiko, ni lazima utafuta kamusi, itafaki, ramani na vitabu vinaoweza kusaidia mafunzo yako. |

## Maneno Machachi Kutoka Mwandishi:

Ni tumaini yangu umejifunza mambo mengi kuhusu Biblia kutoka kitabu hiki. Kama utakuwa na swali au utahitaji msaada ya kiroho naomba utuandika sisi kwenye anwani utaona hapa chini. Pia kama utahitaji masomo ya bure kupitia posta pia tuma jina lako na anwani kwa anwani utaona chini.

Kumbuka hakuna kitabu kingine hapa ulwenguni kimetoka kwa Mungu. Kama utataka kupata wokovu ni lazima ufuata kitabu cha Mungu tu, kwa sababu ndani ya sisi wanadamu hatweai kupata Mungu bila Biblia

Asante.
Ndugu Heath Stapleton

Www.kanisalakristo.com